



Committee to Protect Journalists

## **CPJ yaitaka Burundi kuwaachia huru wanahabari 4 wa *Iwacu* wakati wa rufaa**

Nairobi, Mei 4, 2020 – Kabla ya kusikizwa kwa rufaa ya wanahabari wanne wa mtandao wa habari wa Burundi *Iwacu*, [waliohukumiwa vifungo vya miaka 2.5](#) gerezani Januari, Kamati ya Kuwalinda Wanahabari (CPJ) imetoa taarifa ifuatayo:

“Wanahabari hao wa *Iwacu* hawakufaa kamwe kukamatwa, tuache hata kuhukumiwa kufungwa jela. Huku virusi vya corona vikiendelea kusambaa, kila muda wa ziada wanaokaa kizuizini ni hatari ya zaidi kwa afya yao,” alisema mwakilishi wa CPJ Afrika Muthoki Mumo. “Haiwezekani kufuta dhiki na mateso ambayo tayari wanahabari hao wanne wa *Iwacu* wamepitia, lakini mamlaka zinaweza kusitisha ukiukaji huu wa haki kwa kutopinga rufaa yao na kuwaachia huru mara moja na bila masharti.”

Wanahabari hao wanne – mwanahabari wa redio Christine Kamikazi, mkuu wa kitengo cha siasa Agnès Ndirubusa, mwandishi wa Kiingereza Egide Harerimana, na mpiga picha TERENCE Mpozenzi—wamepangiwa kufika mahakamani kesho Mei 6 kwa kikao cha kusikizwa kwa rufaa yao, mkurugenzi wa *Iwacu* Léandre Sikuyavuga na mwanzilishi Antoine Kaburahe wameambia CPJ kupitia mtandao wa kijamii wa kutuma ujumbe. Wanahabari hao wamekuwa kizuizini tangu Oktoba 2019, na Januari mwaka huu [walipatikana na kosa la kuhujumu usalama wa taifa](#).

CPJ na mashirika mengine 80 ya kutetea haki za wanahabari na haki za kibinadamu hivi majuzi walituma [barua kwa viongozi wa nchi za Afrika](#), kuwahimiza kuwaachia huru wanahabari wote wanaozuiliwa kwa kuzingatia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.